

Waraka wa Maelezo ya Muda wa Ziada Kwa Watoa huduma Binafsi

Ikiwa waraka huu wa maelezo umekusudiwa kusaidia Watoa huduma Binafsi fahamu kanuni kuhusu vikomo vya kazi na muda wa ziada. Tafadhali wasiliana na meneja wa kesi wa mteja au tembelea www.dshs.wa.gov/altsa/IPOT kwa maelezo zaidi.

TAARIFA YA JUMLA YA MUDA WA ZIADA

1. Ni nini wiki ya kazi?

Wiki ya kazi huanza Jumapili 12:00 a.m. (saa sita usiku) na humalizika Jumamosi ifuatayo saa 11:59 p.m.

2. Ni nini Kikomo cha Wiki ya Kazi (WWL)?

WWL ni idadi ya jumla ya masaa ya huduma unayoweza kufanya kazi katika wiki. Sheria ya jimbo la Washington ya mwaka 2016 imeweka kikomo juu ya idadi ya masaa ambayo Mtoa Huduma Binafsi (IP) anaweza kufanya kazi katika wiki ya kazi. Watoa Huduma wote wana kikomo cha wiki ya kazi (WWL). Unaweza kufanya kazi tu hadi kufikia kikomo chako cha WWL ikiwa masaa hayo yameteuliwa kwako na mteja mmoja au zaidi na mteja unaemfanyia kazi anastahiki kupokea masaa hayo. Mteja anaweza asiteuwe zaidi ya masaa yaliyokadiriwa ya kila mwezi katika mpango wake wa Matunzo. WWLs itasaidia kudhibiti gharama za muda wa ziada ili kuhakikisha udhamini wa huduma unaendelea kupatikana kwa wote wanaohitajia huduma hizo.

3. Jinsi gani DSHS huamua WWL yangu ya daima na jinsi gani naweza kujua WWL yangu ya daima?

Sheria ya jimbo ilipitishwa Aprili 2016. Sheria hii iliweka kikomo cha masaa 40 ya WWL kwa watoa huduma wote ispokua wale ambao waliokuwa wanafanyakazi ya wastani wa zaidi ya masaa 40 ya huduma kwa wiki mnamo Januari 2016. Vikomo vya WWLs vya zaidi ya masaa 40 viliamuliwa kwa kugawanya masaa ya Januari 2016 ya kulipwa ya huduma ya mtoa huduma kwa 4.33 na kukaribia robo saa ya karibu zaidi. Mnamo Mei 2016, DSHS ilituma notisi kwa watoa huduma ambao walifanyakazi ndani ya Januari 2016 na taarifa zao za kikomo cha WWL. Hakuna kikomo cha WWL cha daima ambacho kinaweza kuzidi masaa 65. Ikiwa ulianza kufanyakazi kama mtoa huduma baada ya Januari 2016, kikomo chako cha WWL ni masaa 40.

4. Vipi kama nafikiri kikomo changu cha daima cha WWL kiliamuliwa kimakosa?

Ikiwa unafikiri kwamba kikomo chako cha WWL kiliamuliwa kimakosa, unaweza kutuma ombi kwa meneja wa kesi wa mteja na DSHS itakagua masaa yako kulingana na Kanuni Kuu ya Washington 388-114-0050.

5. Je, kikomo changu cha daima cha WWL kitakuja kubadilika?

Ikiwa kikomo chako cha WWL ni kati ya masaa 60.25 na 65, kitapungua hadi masaa 60 mnamo Julai 1, 2017 ispokuwa kukiwa na mabadiliko katika sheria. Vinginevyo, kikomo chako cha daima cha WWL hakitabadilika kwa muda wote unaoendelea kustahiki kama Mtoa huduma. Kikomo chako cha WWL pia kitaendelea kuwa kama kilivyo ikiwa utasitisha huduma na kurejea tena kama mtoa huduma siku za mbele.

6. Ni huduma gani zinajumuishwa katika masaa ya huduma katika kikomo changu cha WWL?

- Huduma ya Matunzo Binafsi
- Huduma ya Matunzo ya Faraja
- Mafunzo ya Kupata Ujuzi
- Huduma ya Matunzo ya Pumziko

7. Je, kikomo changu cha WWL kinahusika na muda wa safari, mafunzo ya DSHS yanayohitajika, au likizo inayolipwa (PTO)?

Hapana. Muda wa safari, mafunzo ya DSHS yanayohitajika, na likizo inayolipwa (PTO) havijumuishwi katika kikomo chako cha WWL. Hio inamaana kwamba unaweza kufanyakazi hadi kikomo chako cha WWL ukifanya kazi kwa mteja huyo kama inavyohitajika, hata katika wiki unazokuwa na mafunzo yanayohitajika, muda wa safari uliothibitishwa, au chukua likizo ya kilipwa (PTO).

Waraka wa Maelezo ya Muda wa Ziada Kwa Watoa huduma Binafsi

MALIPO YA MUDA WA ZIADA (OT)

8. Jinsi gani muda wangu wa ziada unaolipwa unahesabiwa?

Utalipwa mshahara wako wa kawaida kwa muda wote unaofanyakazi hadi masaa 40 katika wiki ya kazi. Kwa muda wote unaofanyakazi zaidi ya masaa 40, utalipwa mara 1.5 ya mshahara wako wa kawaida. Mfumo wa malipo wa IPOne hulipa kiwango kamili cha masaa unayofanya kazi katika wiki ya kazi kwa mshahara wako wa kawaida (hutambulika kama “bei kamili”). Huonyesha muda wa ziada (OT) kama bei ya ziada ya ½ kwa masaa ya ziada. Majumuisho hayo huongezwa pamoja kwa ajili ya malipo ya mwisho.

Mfano:

Umefanya kazi masaa 45 katika wiki ya kazi na bei yako ya kawaida ni \$12/kwa saa.

Malipo yako yatakuwa ni:

Masaa 45 x \$12 kwa saa (bei kamili) = \$540

+ masaa 5 ya muda wa ziada x \$6 (nusu bei) = \$30

Jumla \$540 + \$30 = \$570

Muda wa ziada huonyeshwa katika Maelezo ya Ufupisho wa Malipo na hufanuliwa katika Sehemu ya Mapato. Kwa mfano huu Sehemu ya Mapato itaonyesha masaa 45 ya huduma ya matunzo binafsi na masaa 5 ya muda wa ziada.

9. Je, nitalipwa muda wa ziada kwa muda wa safari, mafunzo ya DSHS yanayohitajika, au likizo inayolipwa (PTO)?

Utalipwa muda wa ziada kwa muda wa safari na mafunzo ya DSHS yanayohitajika ikiwa masaa ya jumla uliyofanyakazi katika wiki ya kazi ni zaidi ya 40. Masaa ya likizo inayolipwa (PTO) hayazingatiwi kama masaa yaliyofanyiwa kazi, kwa hiyo hayastahiki kwa malipo ya muda wa ziada.

TAARIFA KWA IPS AMBAO WANAWA KIKOMO CHA DAIMA CHA WWL CHA MSAA 40

10. Je, naweza kufanyakazi zaidi ya masaa 40 katika wiki ya kazi?

Huenda usiweze kufanya kazi zaidi ya masaa 40 ya huduma katika wiki ya kazi isipokuwa ukipokea muafaka maalum wa mteja kutoka kwa DSHS ili kufanyakazi kwa muda zaidi ya masaa 40.

11. Je, naweza kufanya kazi zaidi ya kikomo changu cha daima cha WWL ikiwa nafanya kazi kwa wateja wengi?

Utalazimika kupangilia masaa yote ya huduma ya mteja ndani ya kikomo chako cha daima cha WWL, bila ya kujali wateja wangapi unawafanyia kazi. Ikiwa unafanyakazi kwa mteja zaidi ya mmoja, utalazimika kupangilia muda wako na kila mmoja wao ili kuhakikisha kwamba, unapojumuisha masaa yako yote ya huduma kwa pamoja, hufanyi kazi zaidi ya kikomo chako cha daima cha WWL.

12. Nini napaswa kufanya ikiwa mteja ninaemfanyia kazi anataka kunipangia nifanyekazi masaa zaidi ya niliyonayo katika kikomo changu cha daima cha WWL?

- Mweleze kwamba huruhusiwi kufanya kazi zaidi ya kikomo chako cha WWL na kwamba kufanya hivyo kutazingatiwa kama kudai kwa ziada. Tazama #19 kwa maelezo zaidi kuhusu kudai kwa ziada
- Usikubali kazi ambazo zitakusababishia kufanya kazi zaidi ya kikomo chako cha WWL.
- Mhimize mteja kutumia mtoa huduma wa ziada.
- Mhimize mteja awasiliane na meneja wake wa kesi ikiwa mteja huyo ni vugumu kwake kuelewa kikomo chako au hawezi kupata mtoa huduma wa ziada.
- Tafadhali tazama #18 katika ukurasa 3 kwa maelezo zaidi kuhusu mahitaji ya dharura na ya haraka.

Waraka wa Maelezo ya Muda wa Ziada Kwa Watoa huduma Binafsi

TAARIFA KWA IPS AMBAO WANAWANA KIKOMO CHA DAIMA CHA WWL CHA MSAA 40.25 AU ZAIDI

13. Je, naweza kufanyakazi zaidi ya masaa 40 katika wiki ya kazi?

Ikiwa umepokea notisi ya maandishi kutoka kwa DSHS kwamba kikomo chako cha daima cha WWL ni zaidi ya 40 au ikiwa umepata muafaka maalum wa mteja wa ongezeko la muda la kikomo, unaweza kufanyakazi hadi idadi ya masaa yaliyopo kwenye notisi yako.

14. Nini napaswa kufanya ikiwa nafanyakazi kwa zaidi ya mteja mmoja?

Tafadhali tazama jibu la swali #11.

15. Je, itakuaje ikiwa mteja ninaemfanyia kazi ananitaka kurekebisha masaa yangu ili kufanyakazi zaidi ya kikomo changu cha daima cha WWL kwa wiki moja?

Unaweza kurekebisha masaa yako ikiwa yote ya yafuatayo ni kweli:

- Mteja ana mahitaji; na
- Kufanyakazi masaa ya ziada hakuzidi masaa ya mteja ya kila mwezi yaliyokadiriwa; na
- Kufanyakazi zaidi katika wiki moja hakutamsababishia mteja kubaki bila ya huduma ya matunzo ya msingi katika wiki nyingine za mwezi huo; na
- Kufanyakazi zaidi katika wiki moja hakutakusababishia kufanyakazi zaidi muda wa ziada katika mwezi huo zaidi ya ambavyo ulipaswa kama ungefanyakazi hadi kikomo chako cha WWL kila wiki ya mwezi huo.

Pale ambapo kikomo chako cha WWL ni zaidi ya 40, unaweza kurekebisha masaa yako kadri inavyohitajika madamu hufanyi kazi zaidi muda wa ziada katika mwezi kuliko ambavyo ungefanya kazi kwa kawaida. Kiwango cha kila mwezi cha masaa ya muda wa ziada kinahesabiwa kwa kutoa masaa 40 kwenye kikomo chako cha WWL na kuzidisha salio na idadi ya Jumamosi za mwezi huo.

Mfano:

Kikomo cha WWL cha Jose ni masaa 46. Kiwango cha muda wa ziada wa kila mwezi wa Jose ambao anaweza kufanyakazi kinategemea na idadi ya Jumamosi za mwezi anaofanya kazi.

Hesabu Jumamosi 5: $46 - 40 = 6 \times 5 = 30$

Hesabu Jumamosi 4: $46 - 40 = 6 \times 4 = 24$

Mteja ambae Jose anamfanyia kazi anamtaka afanyakazi kwa ratiba inayoweza kubadilika ndani ya mwezi mzima, ambapo Jose anaweza akafanya madamu hafanyakazi zaidi ya masaa 30 ya muda wa ziada katika miezi yenye Jumamosi 5, au masaa 24 ya muda wa ziada katika miezi yenye Jumamosi 4.

Pia unaweza kurekebisha masaa yako ili kufanya kazi zaidi kuliko kikomo chako cha WWL ikiwa mteja unaemfanyia kazi atanunua masaa zaidi kwa bajeti yake ya Huduma za New Freedom na Veteran Directed Homecare.

16. Nini napaswa kufanya ikiwa mteja ninaemfanyia kazi anataka kunipangia nifanyakazi zaidi ya masaa ya muda wa ziada ya jumla ya kila mwezi niliyonayo katika kikomo changu cha daima cha WWL?

Tafadhali tazama jibu la swali #12.

KIKOMO MAALUM CHA MUDA CHA MTEJA CHA KAZI CHA KILA WIKI (CSWWL)

17. Ni nini CSWWL ya muda?

Mteja unaemfanyia kazi anaweza kuiomba DSHS iongeze kwa muda kikomo chako cha WWL wakati anatafuta mtoa huduma wa ziada ili kutimiza mahitaji yake. DSHS itakujibu kwa barua ya muafaka ya maandishi au kanusho la maandishi. Ikiwa imeafikiwa, notisi pia itakueleza tarehe ambayo muafaka utaanza na kumalizika na idadi ya masaa yaliyoafikiwa. Mteja unaemfanyia kazi pia atapokea nakala. Ombi/taarifa hii ya maandishi pia inajulikana kama ombi la CSWWL. DSHS haitaafiki kikomo cha muda cha WWL ambacho kinazidi masaa ya mteja yaliyokadiriwa kila mwezi.

Waraka wa Maelezo ya Muda wa Ziada Kwa Watoa huduma Binafsi

MAHITAJI YA DHARURA

18. Nini napaswa kufanya ikiwa nimefanya kazi masaa yote katika kikomo changu cha WWL lakini mteja ana mahitaji ya dharura na ya haraka na lazima niendelee kufanya kazi ili kusadia afya ya mteja au usalama wake?

- Bakia na mteja huyo mpaka hali iwe salama na tulivu.
- Ikiwa kuna dharura ambayo inahitaji huduma za matibabu ya dharura, wasiliana na 9-1-1.
- Maliza siku yako ya kazi haraka sana mara tu inapokuwa ni salama kufanya hivyo.
- Wasiliana na meneja wa kesi siku ya kazi inayofuata ili kueleza tatizo hilo.

KUDAI KWA ZIADA

19. Ni nini kudai kwa ziada?

Kudai kwa ziada hutokea pale:

- Unapofanya kazi masaa mingi zaidi katika mwezi kuliko ulivyoruhusiwa kutoa huduma; au
- Unapofanya kazi masaa zaidi ya kikomo chako cha WWL ambayo hayakuafikiwa na DSHS; na
- Unapodai muda zaidi wa kusafiri kuliko ulivyoruhusiwa kutoa huduma katika wiki ya kazi.

20. Ni nini Madai ya Mkataba?

Madai ya mkataba ni notisi ambayo hutumwa kwako na DSHS. Notisi hio hukuarifu kwamba umefanya kazi masaa ya huduma zaidi ya muda wa ziada au masaa ya muda wa kusafiri kuliko ulivyoruhusiwa kufanya kazi.

21. Nini kitatokea ikiwa nitafanya kazi zaidi ya kikomo changu cha WWL au muda wa kusafiri?

- Kila wakati unapozidisha madai, utapokea notisi ya maandishi ya madai ya mkataba na maelezo kutoka kwa DSHS inayokukumbusha umuhimu wa kutofanya kazi muda wa ziada ambao haujaafikiwa. Notisi hio pia itatumwa kwa mteja ambaye unamfanyia kazi na wawakilishi wake.
- Katika tukio la tatu la kudai kwa ziada, mkataba wako unaweza kuatishwa au unaweza kuwa hustahiki kupokea malipo kwa siku 90. Ikiwa mkataba wako utakatishwa utalazimika kusubiri siku 90 kabla ya kuwa unastahiki kupata mkataba mpya.
- Ikiwa kwa kiasi kikubwa au mara kwa mara unavuka vikomo vyako vya wiki ya kazi au muda wa kusafiri, DSHS inaweza kukatisha mkataba wako kwa kosa hilo na kukataa kuweka mkataba tena na wewe.

22. Je, ni muda gani madai ya mkataba yatabaki kwenye faili langu la mkataba?

Kila dai la mkataba litandelea kubaki wazi kwa miezi 12 kuanzia tarehe ya notisi ya madai ya mkataba. Baada ya miezi 12, dai hilo la mkataba hufungwa.

23. Jinsi gani naweza kuepuka madai ya mkataba?

- Daima panga ratiba yako ya kazi mapema na iandike.
- Ikiwa mahitaji ya mteja yatabadilika na ukalazimika kufanyakazi kwa ratiba nyingine ambayo inaathiri kikomo chako cha WWL, wasiliana na meneja wa kesi wa mteja haraka sana.
- Rekodi muda wako wa kazi kwenye waraka wa kazi baada ya kila siku unayofanya kazi, pia inaweza kusaidia kurekodi muda katika kalenda ya karatasi. Kagua mara nyingi ili kuhakikisha kwamba unabaki ndani ya kikomo chako cha WWL.
- DSHS ina vyanzo vinavyopatikana ili kukusaidia wewe na mwajiri/mteja wako kujifunza zaidi kuhusu kudhibiti ratiba yako ili kubaki ndani ya kikomo chako cha WWL. Vyanzo hivi vinapatikana katika www.dshs.wa.gov/altsa/IPOT.